**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA-RUNGWE**

***Namba za simu***
Mkuu wa shule: 0766-869920
Makamu Mkuu wa Shule: 0755-052550

**Shule ya Sekondari Nkunga,**
S.L.P. 434, Tukuyu.
Tarehe …………...

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………….
…………………………………………….
S.L.P ……………………….
…………………………….
**KUMB.Na**.NKU/SS/S.1644/VOL.01/.........

Jina la mwanafunzi .........................................................

S.L.P ...........................

YAH**: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NKUNGA WILAYA YA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.**

**1.0 UTANGULIZI .**

Nina furaha kubwa kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Nkunga ipo umbali wa kilomita 30 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Rungwe-Tukuyu. Ipo Kaskazini Magharibi mwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe. Unapokuja shule fika mji mdogo wa Kiwira kuna usafiri wa bodaboda stendi ya Igogwe au Karasha,nauli ni shilingi 2500/- mpaka 3000/- umbali wa kilomita saba toka Kiwira.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021.**

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**2.1.SARE ZA SHULE.**

a) Sare ya shule ni suruali mbili (2),rangi ya damu ya mzee na khaki kwa wavulana na sketi mbili (02) rangi ya damu ya mzee na khaki kwa wasichana.Sketi kwa wasichana ziwe **ndefu sana** na linda za kufukuzana na **sio linda boksi** na kwa wavulana mifuko mitatu ;miwili ya ulalo mbele na mmoja nyuma. Hijabu nyeupe kwa waumini wa Kiislamu.

b) Mashati mawili (02) tetroni mikono mifupi.
c) Viatu vyeusi vya ngozi ,vyenye kamba na kisigino kifupi.
d) Soksi nyeupe kwa wasichana ,na nyeusi kwa wavulana jozi mbili .
e) Sare ya michezo.traksuti nyeusi zenye mistari mieupe.
f) Sweta moja (1) rangi ya damu ya mzee.
g) Mkanda wa kiunoni rangi ya damu mzee/mwekundu

**2.2 VIFAA:**

a) Mwanafunzi apatiwe daftari tisa (09) kubwa ,mkebe wa hisabati ,Oxford Dictionary (Kiingereza kwa Kiingereza),faili la plastic springi na Picha za passort mbili (02) ,fagio wa chelewa na mathematical Table ( Four Figures).

**2.3 MAHITAJI YA CHAKULA.**

Mahitaji ya chakula kwa wanafunzi wa kutwa (*day students*). Mpango wa chakula shuleni ni wajibu wa mzazi kumchangia mwanae kupitia kamati.Kila mzazi/mlezi ataelekezwa kikao cha wazazi/walezi.

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro.
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv) Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzake, mwalimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
vi) Kusuka mwenye kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii) Kufuga ndevu.
viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix) Uvutaji wa sigara.
x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi) Kudharau bendera ya Taifa.
xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**4. Baadhi tu ya kanuni za shule**:Ni marufuku tena ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kutenda yafuatayo:-

a. Kuwa bwenini wakati wa vipindi (**adhabu yake ni kurudishwa nyumbani**) kwa wale wa hosteli.
b. Kuwa na nywele fupi haturuhusu kusuka. **Hivyo ni lazima kunyoa nywele .**
c. Kuwa na kucha ndefu ama kuzipaka rangi, kuvaa hereni,bangili, kofia ,mzura na mapambo mengine yoyote hayaruhusiwi kabisa.
d. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

**NB: Kama mwanao hawezi kuishi bila simu ya mkononi, basi hafai katika mazingira ya shule ya sekondari Nkunga na ni vema asifike kabisa shuleni maana atafukuzwa shule mara moja.**

Ni matumaini yangu kuwa mzazi/mlezi wako atashirikiana nasi katika kukuongoza hadi ufanikiwe kuipata elimu ya sekondari ipasavyo.

**5. 0 TAARIFA ZIFUATAZO ZINATAKIWA ZIJAZWE KWA KILA MWANAFUNZI NA KUWASILISHWA MWANAFUNZI ANAPO RIPOTI.**

i) Hati ya Taarifa ya afya ya Mwanafunzi ( Medical Examinaton Form) ijazwe na mgaga mkuu wa Hospitali ya Serikali.
ii) Fomu ya kukili kwa mwanafunzi kuwa tayari kusoma
iii) Fomu ya kukili kwa mzazi/mlezi kuwa tayari kimalezi
iv) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa

v) Namba ya simu ya mzazi/mlezi

MWISHO: **TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO YOTE KWA MAKINI NA KUZINGATIA.**

**KARIBU SANA!**

____________________

**JAMES S LUKOSI**
**MKUU WA SHULE**

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI WA HOSTELI**

a) Mchango wa hosteli **Tsh. 435,000/= (laki nne na thelathini na tano elfu).** mchanganuo wa fedha hii ni.

GHARAMA ZA CHAKULA KWA MWANAFUNZI MMOJA KWA MWAKA **335,000/=.**

| A. | AINA YA CHAKULA | KIASI CHA MLO MMOJA KWA MWANAFUNZI | KWA SIKU | KWA WIKI | KWA MWEZI | KWA MWAKA | TSH. | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | *UNGA (UGALI, UJI)* | $^{1}/_{4}$=0.25kg | 0.36kg | 25kg | 10kg | 100kg | 100kg×1000/=100,000/= | 100,000 |
| 2 | *MCHELE* | $^{1}/_{4}$kg=0.25kg | $^{1}/_{4}$kg | $^{1}/_{2}$ | 2kg | 20kg | 20kg×2000/= 40,000/= | 40,000 |
| 3 | *MAHARAGE* | $^{1}/_{8}$kg=0.125kg | 0.41kg | 1.625kg | 6.5kg | 65kg | 65kg×1400= | 91,000/= |
| 4 | *MAKANDE* | $^{1}/_{4}$kg=0.25kg | 0.25kg | 0.5 | 2kg | 20kg | 20kg×700= | 14,000/= |
| 5 | *NYAMA* | $^{1}/_{8}$kg=0.125kg | 0.125kg | 0.125kg | 0.5kg | 5kg | 5kg×6000= | 30,000/= |
| 6 | *MAFUTA* | 0.0068 lita | 0.0068 lita | 0.0476kg | 0.19 | 1.9kg | 2kg×3800= | 7,600/= |
| 7 | *CHUMVI* | 0.0051kg | x2=0.0102kg | 0.0714kg | 0.2856kg | 3kg | 3kg×1000= | 3,000/= |
| 8 | *MBOGA/MAJANI* | 100/= kwa fungu | 100/= | 4x2=200 | 800/= | 8,000/= | | 8,000/= |
| 9 | *VITUNGUU* | 1.5kg | 1.5kg | 3.0kg | 12.0kg | 1.2kg | 1.2kg×1000= | 1,200/= |
| 10 | *NYANYA* | 15kg | 15kg | 15kg | 60kg | 600kg | 0.6kg×1000= | 600/= |
| 11 | *KUNI* | 48/= | 143/= | 1,000/= | 4000/= | 4000/= | | 40,000/= |
| **JUMLA KUU** | | | | | | | | **335,400/=** |

b) **GHARAMA ZINGINE.**
Matron 50,000/=
Mpishi 20,000/=
Matibabu madogo madogo 10,000/=
Vifaa vya usafi 8,000/=
Ukarabati 12,000/=
**Jumla ni 100,000/=**

c)**AWAMU ZA MALIPO.**
**Januari - Machi** 150,000/-
**April -Juni** 100,000/-
**Julai - Septemba** 100,000/-
**Septemba -Desemba** 85,000/-

Fedha zote zilipwe kupitia **Benki NMB Tukuyu. Akaunti. Na: 61410024801** jina la akaunti **ELIMU YA KUJITEGEMEA NKUNGA SEKONDARI.** Fedha yoyote haita pokelewa shuleni. mwanafunzi anaporipoti na pay slip ambayo atakuwa amelipia michango hiyo ya Hosteli. Na mwanafunzi hatapokelewa kujiunga na hosteli pasipo kulipia michango hiyo ama **kuja na chakula kama kilivyoainishwa katika jedwari hapo juu**.
Ni marufuku kwa wanafunzi yeyote kuwa na simu na nguo za nyumbani kwa watakao kaa hosteli.

d) **MAHITAJI MENGINE**

- mashuka mawili, rangi ya pink 1 na bluu 1 (yasiwe na maua)
- Blanketi moja ( 1)
- Chandarua kimoja size ndogo yenye pembe nne.
- Sukari ya kutosha muhula mmoja (sukari atajitegemea)
- Sabuni ya kuogea na kufulia za kutosha.
- Mswaki na dawa ya meno

- Mafuta ya kupakaa ya kawaida
- Mto (pillow ) mmoja (1)
- Sahani, kikombe, kijiko na ndoo moja ya kufulia na kuogea na taulo moja (1)
- Shamba dress gauni light blue
- Tracksuti nyeusi yenye mistari mieupe na raba ya michezo
- Godoro futi 2 $\frac{1}{2}$
- Sanduku la chuma (tranker)
- Ndoo

**Angalizo**:

1. Hakuna chakula maalum ( special diet)
2. Mtoto atatembelewa na mzazi/mlezi masaa na siku za kazi tuu na sio kwenda moja kwa moja hosteli.

---

**JAMES S. LUKOSI**
**MKUU WA SHULE.**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

P.o Box 434
Tukuyu**.**
Date: ..........................

**PART: A.**
To the medical Officer,
......................................
......................................
......................................
Re: ..............................................................

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time secondary schools studies that may also include physical training the Examination should include the following categories or subcategories which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnant (category IV) will also render girl candidates ineligible for the cause.

1. (a) Eye sight
   (b) Hearing
   (c) Speech
   (d) Limbs
   (e) General disease
   (f) Leprosy
   (g) Epilepsy

Other serious diseases.............................................................................
Pregnancy.............................................................................................

**PART B**: MEDICAL OFFICER.
(To **be completed by a Government Officer**)
I have Examined the above named and consider that he/she is physically fit for a full time secondary studies.

(a) Eye sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Limbs
(e) General disease
(f) Leprosy
(g) Epilepsy.

II. Neuroses.........................................................................................
III. Other serious diseases.......................................................................
IV. Pregnancy.........................................................................................

Date: .............................. Name: ..................................................... Signature..........................

Station................................... Date: